

## Jinsi ya Kushiriki Katika Kamati na Timu za Shule

Familia na walimu wanapofanya kazi pamoja, watoto wana uwezekano mkubwa wa kufanikiwa, kuhudhuria shule kila siku, na kuhisi wameunganishwa na wanafunzi wenzao na walimu. Wazazi na walezi wanaohusika na shule hujihisi kuwa sehemu ya jamii ya shule. Njia moja muhimu ambayo familia fulani huchagua kushiriki katika shule ya mtoto wao ni kwa kujiunga na timu au kamati ya shule. Wazazi na walezi wanaweza kukutana na familia nyingine na kufanya kazi na walimu na wasimamizi ili kufanya maamuzi kuhusu shule au wilaya.

### Ninawezaje kuhusishwa?

#### Hudhuria mikutano ya kikundi cha wazazi.

Katika shule nyingi, kuna vikundi vya wazazi na walezi kukutana pamoja. Katika vikundi hivi, wazazi na wafanyikazi wa shule hujadili mahangaiko yao na kupanga shughuli za kuwasaidia wanafunzi, walimu, na familia zote shuleni. Nyakati nyingine vikundi vya wazazi vinaweza kuzingatia mada au vikundi vya kitamaduni hususa.

Nyakati nyingine kikundi kinaweza kuitwa Chama cha Mwalimu na Mzazi (PTA) au Shirika la Mwalimu na Mzazi (PTO).

#### Jiunge na timu ya uongozi wa shule.

Katika Ohio, kila wilaya ya shule ina timu ambazo hufanya kazi pamoja ili kuboresha shule zao. Timu hizo kwa kawaida hujumuisha wafanyakazi na wasimamizi kutoka shuleni, washiriki wa jamii, na wawakilishi wa familia. Ikiwa una nia ya kuwa sehemu ya timu ya uongozi wa shule, unaweza kumwuliza mwalimu wa mtoto wako, mkuu wa shule, au mzazi mwingine kuhusu fursa zilizo katika shule au wilaya yako.

Wazazi na familia kama yako inaweza kujiunga na timu hizi. Unaweza kushiriki mapendekezo na mawazo muhimu na viongozi wa shule. Wazazi au walezi walio katika timu za shule

huzisaidia shule kufanya maamuzi muhimu. Wao hutegemeza mabadiliko ili kuboresha shule na masomo. Ifuatayo ni habari kuhusu aina za timu unazoweza kupata katika shule yako.

### **Timu ya Uongozi wa Wilaya**

Timu hii inajumuisha wafanyikazi wa shule, washirika wa jamii, na viongozi wa shule. Wao husimamia wilaya ya shule. Timu hii huzingatia mabadiliko yanayoathiri wilaya nzima ya shule.

### **Timu ya Uongozi wa Jengo**

Timu ya uongozi wa jengo hujumuisha wafanyakazi wa shule, walimu, na viongozi wa shule. Viongozi hawa ni pamoja na wakuu na wasimamizi wa shule. Timu hii huzingatia mabadiliko katika shule moja.

### **Timu ya Uingiliaji wa Tabia na Usaidizi Mzuri**

Shule za Ohio zina timu za Uingiliaji wa Tabia na Usaidizi Mzuri (PBIS). Zinafanya kazi na familia na wafanyakazi wa shule ili kuhakikisha kwamba shule inatumia mazoea yanayosaidia ustawi na masomo ya kila mwanafunzi.

## **Ni maswali gani ninayoweza kuiuliza shule?**

- Ni njia gani mbalimbali ninazoweza kuhusishwa katika shule?
- Ni nani ninayoweza kumwuliza kuhusu jinsi ya kuhusishwa katika shule?
- Je, ninahitaji kujua Kiingereza ili kuhusishwa?
- Ninawezaje kujitolea katika shule?
- Ni vikundi gani vya wazazi au familia ninavyoweza kujiunga navyo?

## **Vipi ikiwa sijihisi huru kuzungumza Kiingereza?**

Ni lazima shule ziandae wakalimani kwa ajili ya familia. Wakalimani wanaweza kuzisaidia familia kuzungumza na walimu na wafanyikazi wa shule. Shule pia inaweza kuandaa wakalimani wanaopatikana ili kuzisaidia familia katika matukio ya shule. Unaweza pia kuomba ukalimani au utafsiri kutoka kwa shule bila gharama yoyote. [Jifunze zaidi katika](#)

sehemu yetu ya Kutumia Wakalimani.

### Vifaa vya Ziada

- Kifaa hiki cha Colorin Colorado kinaeleza jinsi wazazi na familia zinaweza kuhusishwa katika shule ya mtoto wao. <https://www.colorincolorado.org/article/parent-participation-how-get-involved-your-childs-school-activities>
- Ukurasa huu wa USA Hello unaeleza jinsi wazazi wanavyoweza kutegemeza elimu ya mtoto wao. <https://usahello.org/education/children/help-child-in-school>
- Mwongozo huu wa Ready4K unahusu kuabiri shule na kuhusishwa katika elimu ya mtoto wako. <https://learn.ready4k.com/school-newcomer-resource>
- Ukurasa huu wa Kuwakuza Wanafunzi wa Lugha huandaa mawazo kuhusu kushiriki katika elimu ya mtoto wako. <https://raisinglanguagelearners.com/ideas-to-participate-in-your-childs-education>

*Vifaa hivi vinalenga kuimarisha ustawi wa kitaaluma, wanafunzi na matokeo ya chuo na kazi kwa wanafunzi wa lugha nyingi wa Ohio. Rasilimali ziliundwa kupitia juhudi ya pamoja kati ya Idara ya Elimu na Kazi ya Ohio (ODEW) na Kituo cha The Ohio State University cha Elimu na Mafunzo ya Ajira (CETE) pamoja na kikundi kilichojitolea cha watetezi wa familia, viongozi wa jamii, wafanyakazi wa wilaya ya shule, na walimu.*